



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 04 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2024/2025.

Mwenyekiti wa Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2024/2025.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

76. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na ucheleweshaji wa asilimia 10 ya mapato ya Serikali za Mitaa yanayotokana na makusanyo ya ndani kinyume na sheria na dhamira ya kuwafikia makundi maalumu yaliyoelezwa katika utaratibu wa 4,4,2.

- (a) Je, tatizo hili unalifahamu vipi.
- (b) Je, ni kweli kuwa pesa hizi bado hazijawafikia walengwa kama zilivyopangwa.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

111. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya maendeleo kwa kutumia mikopo ambayo huikopa kuipitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) au moja kwa moja kwa Benki za nje na wadau wengine wa maendeleo ndani ya nchi. Pamoja na mikopo hii kuleta maendeleo makubwa katika nchi yetu na kuiweshera kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, bado yapo mambo yanayoleta masuali kwa wananchi.

- (a) Je, ni mikopo mingapi na yenye thamani gani iliyokopwa na Serikali tokea mwaka 2020.
- (b) Je, kufikia sasa ni kiasi gani kinakadiriwa kuwa deni la Taifa na ni ongezeko la wastani wa kiasi gani tokea mwaka 2020.
- (c) Je, Serikali imepanga mikakati gani ya kulipa madeni hayo kwa wakati na bila ya kusababisha mzigo mkubwa kwa wananchi.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

214. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni utaratibu gani wa kimkakati unaotumika katika kuteua wachezaji wa timu bora ya Taifa ya Zanzibar pamoja na maandalizi ya ushiriki katika michuano ya kimataifa.

Wizara ya Afya:

238. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tathmini iko vipi juu ya ongezeko na hatua za kinga juu ya maambukizi ya homa ya ini kwa sasa.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

29. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) hutekeleza shughuli zake ikiwa ni pamoja na kuandaa na kusimamia mitihani kwa kutumia fedha wanazopokea kutoka Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

Je, vipi kuhusu upande wa Zanzibar fedha za kuandaa na kusimamia mitihani zinatoka wapi.

198. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni lini Wizara yako itafikiria kwa kina na kuanza ujenzi wa nyumba za walimu, ili kuleta ufanisi na umahiri katika maendeleo ya sekta ya elimu.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

266. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa Mji Mkongwe wa Zanzibar ni miongoni mwa mji maarufu na mashuhuri katika tasnia ya utalii hapa Afrika, hususan katika mwambao wa Afrika Mashariki. Na kwa kuwa mji huu umekuwa ukiathirika mara kwa mara kutokana na athari za kimazingira zikiwemo kupanda kwa maji ya bahari katika maeneo ya makaazi, kuchanganyika kwa maji safi na maji takatifu pamoja na mafuriko siku za mvua kubwa, jambo linalopunguza kwa kiasi kikubwa sifa za mji huu katika medani ya utalii na hatimae kuweza kupelekea kupunguza mapato ya nchi yetu kuititia sekta hii.

Je, kuna hatua zozote za muda mfupi na muda mrefu zilizochukuliwa na zitakazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na changamoto hizo.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

200. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kiasi gani fursa ya uwepo wa teknolojia ya habari na mawasiliano inasaidia kutatua changamoto za kilimo nchini.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Afya:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/2025.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
04 Juni, 2024.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA